EFF'S SURVEILLANCE SELF-DEFENSE

# FARAGHA KWA WANAFUNZI

*https://ssd.eff.org/en/about-surveillance-self-defense*

ELECTRONIC FRONTIER FOUNDATION

LOCALIZATION LAB

Shule zinazidi kutumia teknolojia ya ufuatiliaji ili kuwapeleleza wanafunzi wanapokuwa shuleni, nyumbani, au hata kwenye mitandao yao ya kijamii. Kampuni zinazotengeneza bidhaa na huduma hizi za uchunguzi huzitangaza shulenikama njia ya kudumisha usalama wa wanafunzi–lakini hakuna ushahidi hadi sasa kwamba wanalinda wanafunzi na kwa uhasi zaidi wanaweza kuwadhuru watu wanaopaswa kulinda.

Ufuatiliaji si jambo la kawaida–ni upelelezi. Shule zinazotumia teknolojia hizi kuwafuatilia wanafunzi zinakiuka faragha yao. Iwapo wewe ni mwanafunzi unayepelelezwa na mojawapo ya teknolojia hizi, uko sawa kuwa na wasiwasi.

# Mbinu Zinazotumiwa Kuingilia Faragha Yako

Ingawa si teknolojia zote zinazotumiwa kuwafuatilia wanafunzi zilizo na uwezo sawa, hizi ni baadhi ya mbinu zinazoweza kutumiwa kufuatilia kila kitu unaychofanya na data inayoweza kukusanywa kupitia mbinu hizi. Aina za ufuatiliaji na teknolojia zinazohusiana za uchujaji zinazotumiwa na shule zinaendelea kuongezeka, kwa hivyo orodha hii haijumuishi kila aina ya zana au njia ambazo zingeweza kutumika.

## Aina za Data Zinazoweza Kufuatiliwa

- **Data ya Eneo**: Kufuatilia eneo la wanafunzi kwa kutumia mifumo ya GPS iliyo kwenye kifaa chao, miunganisho ya Wi-Fi na chipu za kielektroniki zilizo katika kadi za basi/vitambulisho, wakiwa ndani na nje ya shule. Shule zimetumia data hii kwa ufuatiliaji na usimamizi wa mahudhurio kiotomatiki, ikijumuisha kuchelewa kwa darasa na kusafiri kwa kutumia basi za shule na kupeana adhabu kama vile kuzuiliwa.
- **Data ya Sauti na Video**: Picha, video na sauti za wanafunzi wanapokuwa kwenye uwanja wa shule. Hizi zinaweza kulinganishwa na hifadhidata za faili za sauti na video zinazojulikana ili kumtambua mtu.
- **Data ya Kuvinjari kwenye Wavuti**: Ufuatiliaji wa historia ya kuvinjari huweka rekodi ya kila kitu unachosoma mtandaoni, kila tovuti unayofikia na kila neno unalotafuta na kisha kusambaza taarifa hii kwa wasimamizi wa shule na ikiwezekana wakaguzi walioajiriwa na kampuni inayotoa huduma ya ufuatiliaji.
- **Matumizi ya Kifaa**: Baadhi ya programu vamizi zinaweza kunasa na kuweka rekodi ya kila kitu unachofanya kwenye kifaa (simu au kompyuta), hata vitu unavyoandika au kufuta. Hii inaweza kujumuisha kila kitu unachotafuta kwenye Mtandao, unachochapisha kwenye mitandao ya

kijamii na ujumbe unaotumwa kupitia programu za gumzo. Ukiingia kwenye tovuti au huduma (kama barua pepe yako au akaunti za mitandao ya kijamii), programu vamizi pia inaweza kunasa majina yako ya watumiaji na manenosiri.

## Aina za Teknolojia Zinazoweza Kukufuatilia

- **Programu ya kupeleleza (wakati mwingine inafahamika kama programu ya ufuatiliaji)**: Hii ni programu ambayo imesakinishwa kwenye kifaa ambayo inampa msimamizi udhibiti wake kamili. Ikiwa zana hii ya ufuatiliaji imesakinishwa kwenye kifaa chako, msimamizi wa programu ya upelelezi anaweza kufikia kila faili, picha, ujumbe mfupi wa maandishi, barua pepe na chapisho la mitandao ya kijamii (hata zile zinazotoweka baada ya muda). Programu hii inaposakinishwa, kifaa kinaweza kufuatiliwa kwa wakati halisi na kuchanganuliwa kwa vitu kama vile data ya eneo, anwani, kumbukumbu za mawasiliano ya simu/jumbe na historia ya kivinjari.
- **Kamera za Ufuatiliaji**: Shule zingine zimeweka kamera za ufuatiliaji ambazo zina uwezo wa kutambua na kufuatilia wanafunzi wanapotembea katika chuo kikuu, ndani ya majengo na nje. Kamera hizi zinaweza pia kuwa na uwezo wa kutambua uso.
- **Vipaza sauti**: Vipaza sauiti vinaweza kusakinishwa katika sehemu mbalimbali shuleni. Vinaweza kuwekwa programu ambayo hutumiwa kurekodi na kuchanganua sauti zote kwa madhumuni ya uchokozi na kutambua hali ya mafadhaiko, lakini mara nyingi teknolojia hii si sahihi.
- **Ufuatiliaji wa Mitandao ya Kijamii**: Hizi ni huduma zinazofuatilia akaunti za mitandao ya kijamii za wanafunzi na kisha kuripoti maudhui yaliyoalamishwa kwa wasimamizi wa shule. Huduma hizi pia zina uwezo wa kuorodhesha watu ambao ni marafiki wa wanafunzi, wanaotangamana nao na mada zinazowapendeza.
- **Ufuatiliaji na Uchujaji wa Mtandao**: Ikiwa unatumia Wi-Fi ya shule, wasimamizi wanaweza kuona kwa kiwango cha juu cha shughuli yako ya kuvinjari wavuti na hata kuzuia ufikiaji wa baadhi ya tovuti. Toleo vamizi zaidi la teknolojia hii linahitaji wanafunzi kusakinisha cheti cha usalama, ambacho huwawezesha wasimamizi kusimbua shughuli za mtandao zilizosimbwa kwa njia fiche za wanafunzi.Cheti cha aina hii kinaposakinishwa, wasimamizi wanaweza kufikia kila kitu ambacho wanafunzi wanasoma na kuandika kwenye vivinjari vyao wanapotumia Wi-Fi ya shule, kama vile maswali kwenye injini za utafutaji, ujumbe unaotumwa kwa wengine na hata taarifa nyeti kama vile manenosiri.
- **Kuchanganua nyaraka na Barua Pepe**: Baadhi ya huduma hujumuishwa na zana za uzalishaji ambazo wanafunzi hutumia kukafanya kazi zao na kuwasiliana na kila mmoja na wafanyikazi wa shule. Ujumuishaji huu

hutumia vichujio kuchanganua maudhui ya kile ambacho wanafunzi huandika katika programu za huduma kama vile Google for Education (pia inajulikana kama G-Suite) na Microsoft's Office 365. Katika hali nyingine, huduma hizi pia huchanganua viambatisho vya barua pepe, kama vile picha au PDF.

**Je, Nini Hutokea kwa Data hii Yote?**

**Ujumlishaji wa Data, Kuripoti na Kushiriki**: Nyingi za huduma na teknolojia hizi huhifadhi data vamizi wanayokusanya kuhusu wanafunzi. Data hii inaweza kusimulia hadithi za kina kuhusu maisha ya mwanafunzi na ina taarifa nyeti sana ambayo inaweza kusababisha madhara makubwa iwapo kuna ufichuzi wa data. Baadhi ya makampuni yanaweza hata kuuza data hii au kuishiriki na wahusika wengine.Katika baadhi ya hali, data ya wanafunzi huripotiwa kwa maafisa wa rasilimali za shule au polisi.

# Je, naweza Kufanya Nini Kuhusu Hilo?

## #1. Fahamu Jinsi Ufuatiliaji wa Shule Unavyokuathiri

Kabla ya kushughulikia ufuatiliaji wa shule, ni muhimu kujua njia ambazo ufuatiliaji huo unaweza kukuathiri wewe na watu walio karibu nawe.

### Je, Wanajua Nini?

Suluhu bora zaidi za kukabiliana na ufuatiliaji hazihitaji kuhusisha zana ya ajabu au suluhisho la keupuka. Wakati mwingine, njia bora zaidi ya kushinda teknolojia ya upelelezi ni kutotumia mifumo inayolengwa na ufuatiliaji (ikiwa unaweza) au kuwa mwangalifu kuhusu maelezo unayofichua unapoendelea kuitumia.

Hatua muhimu katika mchakato huu ni kujua ni teknolojia gani za ufuatiliaji (ikiwa zipo) ambazo shule yako inatumia kukufuatilia, vifaa unavyotumia (vya kibinafsi au vilivyotolewa na shule), na mitandao ya shule. Tafuta na uchunguze ni nini shule inatumia, ili ujue ni taarifa gani inafuatiliwa na uweze kuchukua hatua za kujilinda na kulinda data yako.

### Suala la Faragha kama Kama mchezo wa kushirikiana

Kulinda faragha yako ni kazi ambayo hakuna mtu anayeweza kuifanya peke yake. Ingawa kuna hatua nyingi unazoweza kuchukua ili kulinda faragha yako mwenyewe, ulinzi wa kweli huja tunapolinda faragha ya kila mmoja wetu kama kikundi. Ukibadilisha zana na tabia yako mwenyewe, lakini wanafunzi wenzako

wasifanye hivyo, kuna uwezekano mkubwa kwamba taarifa zinazokuhusu zitanaswa katika ufuatiliaji ambao pia unawafuatilia.

Hebu tutumie mfano wa hali halisi ili kuchunguza jinsi hili linavyoweza kutokea:

*Unatangamana na marafiki kutoka shule yako na wengine wanaosoma shule zingine. Ulizima ufuatiliaji wa eneo kwenye kifaa chako cha mkononi, lakini marafiki zako hawakufanya hivyo. Vifaa vyao hufuatilia kila mahali wanapoenda na muda wanaokaa. Mmoja wa wanafunzi wenzako anawapiga picha wanafunzi wote kwa kutumia simu yake. Kwa kuwa simu yake ya rununu inafuatilia mahali walipo, habari hiyo huingizwa katika metadata ya picha. Rafiki yako anaweka picha hiyo kwenye ukurasa wake wa kijamii na kukutaja. Ikiwa shule yako inafanya ufuatiliaji wa mitandao ya kijamii, wanaweza kuona ni nani aliyechapisha picha, kila mtu aliye kwenye picha hiyo na wakati na mahali ambapo picha ilipigiwa. Ingawa ulijaribu kujizuia ili usifuatiliwe, shule yako sasa inajua maelezo haya yote–sio kukuhusu wewe tu, bali kuhusu kila mtu katika kikundi chako cha marafiki aliyekuwa hapo.*

Uko salama tu kama mtu aliye katika kikundi chako cha kijamii aliye na ulinzi dhaifu zaidi. Ndiyo maana ni muhimu kusaidiana na kulinda faragha yenu kama kundi.

Huenda ukajiuliza, “Maelezo yaliyokusanywa katika hali hii yanawezaje kutumiwa kunidhuru mimi au marafiki zangu?” Angaia baadhi ya mifano ifuatayo:

- Marafiki zako ambao hawaendi kwenye shule unayosomea sasa wamejumuishwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji wa shule yako na hawajui kuwa wamefuatiliwa.
- Huenda wewe na marafiki zako mlikuwa mnahudhuria tukio la jamii za LGBTQ+ wakati picha ilipigwa. Ukishiriki au kujadili picha hii kwenye mitandao ya kijamii ukiwa chini ya ufuatiliaji wa shule, huenda ikaanzisha orodha ya maneno muhimu ya teknolojia ya kuchanganua na kuwaarifu wakuu wa shule. Ikiwa maafisa wa shule wana ubaguzi dhidi ya watu wa jamii za LGBTQ+–au ikiwa shule itawapa wazazi wasiounga mkono suala hili ufikiaji wa maelezo haya kupitia dashibodi, "parent login" au hata arifa za moja kwa moja–hili linaweza kukuhatarisha wewe au rafiki yako.
- Huenda unafanya shughuli za kupanga kisiasa kwa sababu fulani na ikiwa uko katika shule ya kibinafsi au ya kidini, shule na/au wazazi wako wanaweza kosa kuidhinisha suala hilo. Katika hali hii, shule yako inaweza kukufukuza kwa muda au wazazi wako wanaweza kukuadhibu kwa shughuli hii.

## #2. Zungumzia Jambo Hilo

- **Zungumza na Marafiki Wako**: Wasaidie waelewe tatizo hilo, kwa nini ni muhimu kulinda faragha yao na kwamba faragha ni jitihada ya pamoja.
- **Zungumza na Watu Wazima Unaowaamini**: Waeleze wasiwasi wako na uombe usaidizi wao.
- **Tumia maoni yenu ya pamoja**: Iambie shule yako jinsi ufuatiliaji unavyokuathiri. Omba, angalau, uwazi na uwajibikaji kuhusu maamuzi kuhusu teknolojia ya ufuatiliaji shuleni: shule yako inapaswa kuwa na uaminifu kuhusu ni teknolojia inazotumia, jinsi teknolojia hizoz inavyofanya kazi na jinsi data inavyolindwa. Unapaswa pia kuwaambia watoe uthibitisho kwamba teknolojia husaidia kuboresha usalama wa shule na wanafunzi. Unaweza hata ukataka shule yenu ikome kutumia teknolojia fulani kabisa au kuahidi kutotumia teknolojia fulani katika siku zijazo.
    - Kutana na mkuu wa shule yako, msimamizi wa teknolojia ya habari na wasimamizi wengine wa shule.
    - Hudhuria mikutano ya bodi ya shule na uwasilishe wasiwasi wako.
        - Tafuta kalenda ya mikutano ya bodi ya shule yako au wilaya.
        - Husisha wanafunzi wengine na uwe na hoja wazi za kuzungumzia.
        - Zungumza wakati wa kipindi cha kutoa maoni kuhusu mada ikiwa iko kwenye ajenda au katika kipindi cha kutoa maoni ya jumla ikiwa mada haipo kwenye ajenda (fika mapema na uketi karibu na upande wa mbele ili upate nafasi nzuri ya kuzungumza).
        - Uwe jasiri na ukakamavu. Ni faragha yako, sio yao.
    - Fanya utafiti na uandike kuhusu suala hilo kwenye gazeti la shule yako au vyombo vingine vya habari vya wanafunzi.
    - Andaa kesi na uwashirikishe wanafunzi wenzako.
    - Wasiliana na maafisa wa serikali/jimbo na uwaombe wachukue hatua ili kuilinda faragha yako.

### Hoja Unazoweza Kukumbana nazo

Watetezi wa ufuatiliaji hutumia hoja chache za kawaida kukushawishi kuacha kupigania faragha yako. Hapa kuna hoja unazoweza kutumia ili kupinga utamaduni wa ufuatiliaji na kuwasaidia wengine kuelewa madhara ambayo ufuatiliaji unaleta.

## Hoja potofu ya 1. "Ikiwa hukufanya chochote kibaya, huna chochote cha kuficha."

Hoja hii inatokana na dhana isiyo sahihi: kwamba watu "wabaya" tu au watu waliovunja sheria au masharti wanataka faragha. Kuna sababu nyingi za kwa nini mtu angependa kudumisha faragha yake. Suala kuu ni: je, unataka kulinda nini?

Ukweli kwamba ulienda katika kliniki ya afya au ulihudhuria mkutano wa kisiasa, ulitafuta mtandaoni taarifa zinazohusu mwelekeo wa kijinsia au suala la afya au ulishiriki picha za kibinafsi na rafiki - hii yote ni mifano ya mambo ambayo ni ya kibinafsi na yanapaswa kubaki hivyo. Faragha ni kulinda mambo ambayo ni muhimu kwako.

**Hoja potofu ya 2. "Una wasiwasi kwamba *tunaweza* kutumia teknolojia hii kusababisha madhara makubwa, lakini hatutafanya hivyo kamwe!"**

Watu wanaosimamia teknolojia ya ufuatiliaji wanataka uamini kwamba, ingawa wanaweza kutumia teknolojia za ufuatiliaji kutumia vibaya mamlaka yao, hawatafanya hivyo. Si suala la kuaminiana–hawapaswi kuwa na mamlaka haya kwanza. Hii hapa ni filamu fupi inayoonyesha athari ambazo ufuatiliaji unaweza kuwa nazo kwa watu, ikiwa na mifano ya jinsi ukosefu wa usawa wa mamlaka sio haki. Suala lingine ni kwamba data ya wanafunzi mara nyingi iko mikononi mwa kampuni zinazotoa bidhaa na huduma hizi za ufuatiliaji, ambazo zina udhibiti wa data hii nyeti na zinaweza kuiishiriki na wengine.

**Hoja potofu ya 3. Ni kwa ajili ya usalama wako mwenyewe."**

Hakuna ushahidi kwamba teknolojia hizi huongeza usalama wa wanafunzina, kwa kweli, zimeonyeshwa kuwadhuru wanafunzi walewale ambao zimekusudiwa kuwalinda:

- Watu wanapofuatiliwa kila mara, tabia zao hubadilika. Hawajisikii vizuri kujidhihirisha wao wenyewe na mara nyingi hujidhibiti kwa sababu kufuatiliwa kunawafanya waogope.
- Ufuatiliaji huvunja imani ambayo wanafunzi wanayo kwa walimu wao, shule zao na miongoni mwao wenyewe. Wanafunzi wanapohitaji usaidizi, wanaogopa sana kuwasiliana na mtu yeyote ambaye angeweza kuwasaidia kwa sababu ya ukosefu huu wa uaminifu.
- Wanafunzi waliotengwa mara nyingi hulengwa kwa njia isiyofaa na kuadhibiwa kwa sababu ya ufuatiliaji huu usiofaa na usiokuwa na msingi.

**Hoja potofu ya 4. "Haina maana kupinga ufuatiliaji."**

Hofu ya faragha na hisia ya kutokuwa na uwezo ni *jinsi* watetezi wa ufuatiliaji wanavyotaka ujihisi. Hata hivyo, una uwezo wa kuleta mabadiliko. Watu wanapofanya kazi pamoja ili kupigania kile wanachoamini, hufanikiwa. Usiruhusu mtu yeyote akuambie kinyume na hilo.

## #3.Punguza Data Inayofuatiliwa

Ufuatiliaji unahusu kupata habari nyingi iwezekanavyo zinazokuhusu: tabia zako, mahali unapokwenda na wakati unapoenda, watu unaoshirikiana nao na mambo unayojali. Wakati mikakati iliyoelezwa hapa chini haitakulinda kutokana na aina zote za ufuatiliaji zilizoelezwa katika mwongozo huu, itakusaidia kupunguza kiasi cha data ambayo inaweza kukusanywa kukuhusu.

**Ziba Utambulisho wako Mtandaoni**

- Jilinde kwenye mitandao ya kijamii:
  - Unapoweza, badilisha akaunti zako za mitandao ya kijamii ziwe za faragha badala ya akaunti za umma na ukague maombi yote mapya ya wanaokufuata kabla ya kuyaidhinisha. Unaweza pia kutaka kukagua watu wanaokufuata kwa sasa ili kuhakikisha kuwa unawajua na unawaamini.
  - Ikiwa unahitaji akaunti ya umma, zingatia kutumia akaunti tofauti ya faragha kwa mada, machapisho au mazungumzo ambayo ungependa kuweka faragha.
  - Usibadilishe tu mipangilio na tabia yako ya mitandao ya kijamii. Zungumza na marafiki zako kuhusu data inayoweza kuwa nyeti mnayofichua kuhusu kila mmoja wenu mtandaoni na jinsi mnavyoweza kulindana kama kikundi.
  - Punguza hatari unazokabiliana nazo katika vikundi vya mtandaoni kwa kurekebisha mipangilio ya mwonekano.
- Wezesha uthibitashaji wa hatua mbili (au "2FA") kwenye akaunti nyingi za mtandaoni uwezavyo. Ikiwa data iliyokusanywa kukuhusu kupitia ufuatiliaji itafichuliwa kwa ukiukaji, kuwezesha 2FA kutafanya iwe vigumu kwa wengine kufikia akaunti zako, hata kama wanajua majina yako ya mtumiaji na manenosiri.

**Zima Huduma ya Ufuatiliaji wa Eneo Wakati Hauhitaji**

Njia ya kufanya hivyo inaweza kutofautiana kulingana na kifaa na programu. Unaweza kubadilisha mapendeleo yako ya jumla ya kufuatilia eneo katika mipangilio ya mfumo wako, lakini hii inaweza isizime kabisa ufuatiliaji wa eneo. Kwa mfano, baadhi ya programu za simu za rununu zinaweza kuwasha ufuatiliaji wa eneo lako kwa sababu mbalimbali; unaweza kuhitaji kuangalia mipangilio ya simu yako au katika hali nyingine ruhusa za kila programu ili kuizima.

**Jihadhari na Hatari katika Mazingira ya Kibinafsi ikilinganishwa na Mazingira ya Shule**

Kwa wanafunzi walio na wasiwasi kuhusu ufuatiliaji wa shule, ni muhimu kutenganisha maisha yako ya kibinafsi na ya shule. Epuka kutumia vifaa vya

shule, akaunti na mitandao kwa shughuli za kibinafsi. Hata kama shule yako inadai kutumia mfumo wa *geofencing* ( yaani , unafuatiliwa tu ukiwa uko kwenye chuo kikuu), taarifa nyingi zinaweza kufichuka kati ya maisha yako ya kibinafsi na ya shuleni kupitia shughuli zako za Mtandao au vifaa unavyotumia.

- **Vifaa na Mitandao**: Kila kitu unachofanya kwenye *kifaa kilichotolewa na shule*, hata kama unatumia Wi-Fi yako ya nyumbani au mtandao mwingine unaoamini, kifaa hicho kinaweza kufuatiliwa. Vile vile, ikiwa unatumia kifaa cha kibinafsi kwenye *mtandao wa shule*, shughuli zako zinaweza pia kufuatiliwa. Ndiyo maana ni bora kutumia akaunti yako ya kibinafsi au nyeti *tu* kwenye vifaa vyako vya kibinafsi na mitandao unayoamini pekee. Huenda hili lisiwezekane kila wakati, lakini ni lengo zuri.
- **Vitambulisho vya akaunti**: Usitumie barua pepe ya shule yako katika akaunti zozote za kibinafsi za mtandaoni. Hii inaweza kufichua arifa, jumbe za moja kwa moja na maudhui mengine kutoka kwenye akaunti zako za kibinafsi hadi kwenye mifumo ya ufuatiliaji ya shule.
- **Kuvinjari kwenye Wavuti**: Ikiwa kuna habari ambazo hutaki shule yako ifuatilie, ni bora kutafuta mada hizo bila kutumia vifaa na mitandao ya shule.

**Tumia Mbinu Nzuri za Usalama wa Kidijitali**

- Tunza data yako vyema kwa kutumia usimbaji fiche kwenye vifaa vyako.
- Tumia kidhibiti cha nenosiri ili kutengeneza nenosiri dhabiti.
- Amua unachotaka kulinda na uchague zana zinazokufaa.

# Na Mwisho ...

Ufuatiliaji sio jambo la kawaida na sio sawa. Una haki ya kuhisi una wasiwasi na unataka kuzungumza juu ya faragha yako. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi unavyoweza kujilinda, angalia miongozo mingine ya Kujilinda Dhidi ya Ufuatiliaji. Ikiwa unahitaji mwongozo wa kukusaidia kuanza, angalia kifurushi chetu cha Security Starter Pack au orodha yetu ya miongozo ya Vijana wa jamii za LGBTQ.